# JUMUIYA YA ROZARI HAI ULIMWENGUNI –TANZANIA KWA NJIA YA MTANDAO

# NOVENA YA WAFANYAKAZI WOTE KWA MT. YOSEFU MFANYAKAZI

## TAREHE 22-30/APRIL/2020

1.Sala ya Mwanzo Mbele ya Msalaba na ama pamoja na kielelezo cha picha ya Mt. Yosefu.

…Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu.Amina

…Sali sala ya Uje Roho Mtakatifu au wimbo wa Uje Roho Mtakatifu..

SALA YA MWANZO

Uje Roho Mtakatifu uzinee roho za waumini wako, washa ndani moto wa mapendo yako, peleka roho wako, vitaumbwa upya na nchi zitageuka.

Tuombe: Ee Mungu uliyependa kuzifurahisha nyoyo za waumini wako ukiwaletea mwanga wa Roho Mtakatifu, tunaomba tuongozwe na yule Roho, tupende yaliyo mema , tupate daima faraja zake. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu bwana wetu. Amina.

2.SALA YA KUOMBA MSAADA KATIKA KUSALI

Ee Mungu, nimeona mara nyingi kuwa siwezi kusali, napengine sisali.Pengine niko mvivu kwa sala, pengine nataka sana kusali, lakini naona kuwa sina la kusema, niko mkavu kabisa.Ninakuomba, Bwana, unipe moyo mpya ukiniondolea yote yenye kunizuia kusali, hasa uvivu, wasiwasi na elekeo la kushughulika bila mwisho.Uuimarishe utashi wangu ili mara kwa mara nitulie mbele yako na hivyo kuukiri ukuu wako maishani mwangu.

Na mara zile nitakapojiona mkavu katika sala, unisaidie nisikate tamaa mara, bali nielewe kwamba rohoni mwangu ni pa Roho Mtakatifu mwenye kusali ndani yangu. Ninakuomba hayo kwa jina la Mwanao Yesu.-Amina.*(Kitabu cha Twende kwa Bwana Uk.3-4)*

3.SALA YA SIKU HUSIKA.

4. SALI LITANIA YA MT. YOSEFU

Waweza ipata kati ya mojawapo ya Vitabu Vifuatavyo:

1.Chuo Kidogo cha Sala Uk. 45-47

2.Mkusanyiko wa Sala za Maombi Uk.121

3. Sala na Novena Mbalimbali Uk.175-176

4.Mbona mnalala? Kesheni nami. Uk. 65-66

5. Jumamosi ya Kwanza ya Mwezi Sala na nyongeza Uk. 25-27

6. Sala za Utume wa Fatima Uk. Uk. 58-59

7.Twende kwa Bwana Uk. 61-64

8. Hazina ya sala Uk. 141-143

9.Mtandaoni .....

10. Nakadhalika, kwa kutaja baadhi.

5. KUMBUKA KWA MT. YOSEFU

Hii pia utaikuta kwenye;

1. Huruma ya Mungu.Uk. 103
2. Mawaridi ya Sala. Uk. 17
3. Nguvu ya Sala. Uk. 3
4. Kwakutaja baadhi.

   *Kumbuka kwa Mt. Yosefu*

   Ukumbuke, ee Mume safi sana wa Maria na mlinzi wangu mpenzi Mtakatifu Yosefu, kuwa haijasikilika kamwe kwamba ulimwacha yeyote aliyeomba ulinzi na msaada wako.

   Kwa matumaini haya nakujia na kujikabidhi kwako kwa moyo wangu wote .Ee Baba Mlishi wa Mwokozi, usikatae sala yangu bali uipokee kwa wema na uijibu. Amina. *(Kitabu cha Huruma ya Mungu, Ujumbe na Ibada Uk.103)*

*6.SALA YA MWISHO; Tunakimbilia Ulinzi wako.......*

**SIKU YA KWANZA** ***(Jumatano) 22/04/2020***

Baba Yosefu, ulimfundisha Yesu jinsi ya kusali, kucheza na kufanya kazi, utusaidie kutambua kwamba tunaweza kupata elimu kwa kusikiliza na kujifunza. Tukiwa na wewe ambaye unatusaidia na kutuongoza, tunaomba, ee Mt. Yosefu, utuombee tuchague njia sahihi na tubaki kuwa waaminifu katika mafundisho ya Yesu. Amina.

Ee Mt. Yosefu Mfanyakazi, leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako nijaliwe ***(………..Hapa taja Ombi lako)***

*Baba Yetu x 3*

*Salaam Maria x 3*

*Atukuzwe Baba x 3*

**SIKU YA PILI** ***(Alhamis) 23/04/2020***

Mt. Yosefu, ulimwokoa na kumhudumia Neno wa Mungu, na chakula cha uzima kilichoshuka kutoka mbinguni. Uwaangalie mapadri wa Kanisa, ambao asili yao ni nyumba uliyoiongoza, na uwaombee ili nao pia, waweze kuwahudumia kwa uvumilivu watu waliowekwa chini ya uangalizi wao. Tunaomba mapadri wawafundishe kiaminifu waamini Neno la Mungu na kuumega mkate, wa uzima kila siku, kwa ajili yao.Tunaomba wawaimarishe katika imani na matumaini, wakiwafariji katika magumu na katika nyakati za kukukatisha tamaa.Pia umuombe Yesu wetu awavishe taji kwa kazi zao na utumishi wao kwake hapa duniani kwa kuwashirikisha uzima wa milele pamoja nawe Mbingguni milele na milele.Amina

Ee Mt. Yosefu Mfanyakazi, leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako nijaliwe ***(………..Hapa taja Ombi lako)***

*Baba Yetu x 3*

*Salaam Maria x 3*

*Atukuzwe Baba x 3*

**SIKU YA TATU** ***(Ijumaa) 24/04/2020***

Mt. Yosefu Mwenyeheri, sala zako zinaweza kufanya mambo yasiyowezekana, yakawezekana.Ninakuomba uje kunisaidia katika shida na magumu niliyonayo sasa. Uweke kwenye ulinzi wako shida na mahangaiko yangu ninayoyaleta kwako na uniombee, ili niweze kupata msaada kadiri ya mapenzi ya Mungu.
Baba yangu mpendwa, ninakutegemea kabisa, na kwa imani, ninajikabidhi kwako kama mtoto mdogo aliyelala mikononi mwa baba yake. Isisemekane kamwe, kwamba nimekuomba bila mafanikio. Yesu na Maria hawawezi kukukatalia chochote unachowaomba. Kwa matumaini hayo, nakuomba udhihirishe wema na Upendo wako mkubwa kama ilivyo nafasi yako kwa mchumba wako, Bikira Maria, na Mwanao Yesu . Amina

Ee Mt. Yosefu Mfanyakazi, leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako nijaliwe ***(……….Hapa taja Ombi lako)***

*Baba Yetu x 3*

*Salaam Maria x 3*

*Atukuzwe Baba x 3*

SIKU YA NNE *(Jumamosi) 25/04/2020*

Mpendwa Mt. Yosefu, wewe ni msimamizi wa familia ya kanisa .Mungu alikuteua uwe kiongozi na mlinzi wa Familia Takatifu ya Nazareti. Ulichagua kufanya kazi ya useremala, amabayo iliwafanya baadhi ya watu waulizane juu ya Yesu wakisema; "Huyu amepata wapi hekima hii na miujiza hii? Huyu si mwana wa seremala?" Tunaomba kwa sala zako, uwabariki na kuwatia moyo mafundi seremala wote ambao kazi zao ni sawa na ya kwako. Amina

Ee Mt. Yosefu Mfanyakazi, leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako nijaliwe ***(……….Hapa taja Ombi lako)***

*Baba Yetu x 3*

*Salaam Maria x 3*

*Atukuzwe Baba x 3*

SIKU YA TANO *(Jumapili) 26/04/2020*

Mt. Yosefu, Mwenyeheri, mume wa Bikira Maria, uwe nasi katika siku hii ya leo. Ulimlinda na kumthamini Bikira Maria. Ukimpenda mtoto Yesu kama mwano wa kumzaa, ulimwokoa kutoka katika hatari ya kifo. Ulilinde Kanisa, nyumba ya Mungu, lililokombolewa kwa damu ya Yesu. Mlinzi wa familia Takatifu, uwe nasi

katika majaribu. Tunaomba utuombee tujaliwe nguvu ya kuziepuka dhambi na kuzishinda nguvu za dhambi ili katika maisha tuweze kukua katika utakatifu na baada ya kufa, tuvikwe taji la ushindi na kufurahia milele na milele. Amina.

Ee Mt. Yosefu Mfanyakazi, leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako nijaliwe ***(..........Hapa taja Ombi lako)***

*Baba Yetu x 3*

*Salaam Maria x 3*

*Atukuzwe Baba x 3*

SIKU YA SITA *(Jumatatu) 27/04/2020*
Ee Mt. Yosefu, ambaye ulinzi wako ni mkubwa, wenye nguvu na wa haraka mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, ninakukabidhi mahitaji na haja za moyo wangu. Ee Mt. Yosefu unisaidie kwa maombezi yako yenye nguvu na uniombee kwa Mungu anipatie Baraka zote za kiroho kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ili kwa nafasi yako Mbinguni niweze kumsifu na kumheshimu Baba Yetu wa milele. Ee Mt. Yosefu, kamwe sitachoka kukufikiria wewe ukiwa umembeba Yesu, akiwa amelala mikononi mwako.Sithubutu kumsogelea akiwa amepumzika hivyo karibu na moyo wako. Ninakuomba umguse kwa jina langu na kwa niaba yangu, umbusu, umuombe nae anibusu wakati nitakapovuta pumzi yangu ya mwisho. Mt. Yosefu, msimamizi wa walio kufani, utuombee.Amina.
Ee Mt. Yosefu Mwenyeheri, mlinzi mwaminifu wa mabikira, ambaye Mungu amekukabidhi Yesu na Maria uwalinde, ninakuomba, kwa upendo wako kwao, ututunze na kutulinda dhidi ya hatari, uchafu na uovu wa roho na mwili, ili siku zote niwatumikie kitakatifu na kwa upendo kamili.Amina.
Ee Mt. Yosefu, baba mlishi wa Yesu Kristo na mume wa Bikira Maria, utuombee sisi na wale wote watakaofariki siku ya leo (au usiku huu).Amina

Ee Mt. Yosefu Mfanyakazi, leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako nijaliwe ***(..........Hapa taja Ombi lako)***

*Baba Yetu x 3*

*Salaam Maria x 3*

*Atukuzwe Baba x 3*

**SIKU YA SABA** ***(Jumanne) 28/04/2020***

Ee Mt.Yosefu, mfano wa wote wanojituma kufanya kazi, unijalie neema ya kufanya kazi kwa moyo wa toba kwa malipizi ya dhambi zangu nyingi; kufanya kazi kwa bidii kwa kuweka mbele upendo wa kufanya kazi; kuliko vionjo vyangu; kwa shukrani na furaha, kuona ni heshima kutumia na kukuza zawadi nilizopewa na Mungu, kwa njia ya kufanya kazi kwa utaratibu, amani na kwa kiasi na uvumilivu, pasipo kulegea kwa uchovu, au ugumu wa kazi; zaidi ya yote, kwa nia njema kabisa na kujikana mwenyewe, nikikumbuka daima kifo na maelezo ninayotakiwa kuyatoa kwa muda niliopoteza, talanta nilizofukia, mema amabyo sijayatenda na kujiona sana katika mafanikio, kitu amabcho ni hatari katika kazi ya Mungu. Yote kwa Yesu, Yote kwa Maria, yote kufuata mafano wako, ee Baba wa imani Mt. Yosefu! Hii itakuwa ndio kaulimbiu yangu maishani mwangu na milelele. Amina

Ee Mt. Yosefu Mfanyakazi, leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako nijaliwe ***(……….Hapa taja Ombi lako)***

*Baba Yetu x 3*

*Salaam Maria x 3*

*Atukuzwe Baba x 3*

**SIKU YA NANE** ***(Jumatano) 29/04/2020***

Ee Yosefu mwenye heri, tunakimbilia kwako katika masumbuko yetu; na kisha omba shime ya Mchuma wako mt. tunaomba pia kwa matumaini usimamizi wako.

Kwa ajili ya mapendo uliyompenda Bikira Mt. mzazi wa Mungu, na kwa ajili ya kumtunza mtoto Yesu, twakuomba sana, utuangalie kwa wema siye tuliokuwa fungu lake Yesu Kristo, tukakombolewa kwa damu yake. Tusimamie katika masumbuko yetu kwa enzi na shime yako.

Ee mlinzi amini wa jamaa takatifu, uwakinge watoto wateule wa Yesu Kristo. Ee baba uliyetupenda mno tuepushe na kilema chochote cha madanganyo na upotevu . Ee kinga yetu mwezaji, utusimamie huko juu mbinguni ulipo, tunaposhindana na wenye nguvu wakaao gizani.

Kama vile siku za kale ukamwopoa mtoto Yesu katika hatari ya kuuawa, na leo hivi likinge kanisa takatifu la Mungu katika mitego ya adui, na katika shida yote, Mtunze

daima kila mmoja wetu kwa mfano wako, ili tupate msaada wako, kukaa na utakatifu maisha , kufa kifo chema , na kupata mbinguni makao ya raha milele. Amina

### SIKU YA TISA *(Alhamis) 30/04/2020*

Mt. Yosefu, unitazame, mimi niliyekuchagua wewe leo hii uwe msimamizi wangu wakati wa uhai wangu na katika saa ya kufa kwangu. Unitazame na kunizidishia moyo wa sala na wa kumtumikia Mungu.Ufukuze mbali nami kila aina ya dhambi, uniombee ili kifo kisinijie nikiwa sijajiandaa, bali nipate muda wa kutubu dhambi zangu zote kwa njia ya sakramenti ya kitubio katika hali ya majuto kamili, ili saa ile ya kufa kwangu niikabidhi roho yangu mikononi mwa Yesu na Maria. Amina.

Ee Mt. Yosefu Mfanyakazi, leo ninakuja mbele yako, nikiomba kwa maombezi yako nijaliwe ***(……….Hapa taja Ombi lako)***

*Baba Yetu x 3*

*Salaam Maria x 3*

*Atukuzwe Baba x 3*

### SALA YA MWISHO IJUMAA 01/05/2020.

Ee bwana wangu Yesu kristo, naleta maombi yangu maalum kwako ingawa hayatimizi kamwe kwa ukamilifu mahitaji yangu na matamanio mengi yaliyomo moyoni mwangu. Siombi kutimiziwa tu maombi yangu hayo bali Neema ya kukutegemea wewe katika kutimiza kiu ya mahitaji na matamaniao ya moyo wangu ulivyonipatia wewe.

Nakuomba Bwana Yesu ujibu sala na maombi ya waja wako walioungana nami katika kusali Novena hii. Nakuomba uwabariki kwa pendo lako na uwatakatifuze. Nakuomba kwa moyo wangu ulio wazi kabisa nikijua kuwa haitanifaidia chochote nikivipata vya ulimwengu huu na kuipoteza nafsi yangu.

Ee bwana Yesu Kristu, nisaidie daima kuona wema na utukufu wako katika majaribu yangu yote. Nisaidie pia kuona Baraka zako kila siku na daima kukupenda zaidi na zaidi .Asante bwana Yesu kwa kila kitu kwangu. Amina

SHUKRANI YA NOVENA HII.

Chagua sala ama tendo la kiibada Kumshukuru Mungu siku 3*(Mf. Nia ya Misa Takatifu, Kuabudu Ekaristi Takatifu, Rozari Takatifu/ya shukrani, Zaburi, Baba Yetu, Salam Maria, atukuzwe n.k)*

Novena hii inapatikana katika kitabu cha Sala na Novena Mbalimbali.

Imeletwa kwako na Fortunata R. Masaka-Mratibu Rozari Hai Mtandaoni.